

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI



TAARIFA KWA UMMA

UTEUZI WA WAKURUGENZI WATENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJI

Kwa mamlaka aliyo kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019, Waziri wa Maji, **Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa**, amefanya uteuzi wa Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira kama ifuatavyo:

1. **Eng. Ndele Mengo** ameteuliwa kuwa **Mkurugenzi Mtendaji** wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Jijini Mbeya (Mbeya UWSSA). Eng. Mengo anachukua nafasi ya Eng. Simon Shauri ambaye amemaliza muda wake. Kabla ya uteuzi huu, Eng. Mengo alikuwa Meneja wa Ufundu katika mamlaka hiyo.
2. **Eng. Aron Joseph** ameteuliwa kuwa **Kaimu Mkurugenzi Mtendaji** wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Moshi (MUWSA) kuchukua nafasi ya Bi Joyce Ally Msiru ambaye amemaliza muda wake. Kabla ya uteuzi huu, Eng. Joseph alikuwa Mkurugenzi wa Idara ya Uzalishaji na Usambazaji Maji katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi na Usafi wa Mazingira Jijini Dar es Salaam (DAWASA).
3. **Eng. Justine Gordian Rujomba** ameteuliwa kuwa **Kaimu Mkurugenzi Mtendaji** wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Jijini Arusha (AUWSA) kuchukua nafasi ya Eng. Ruth Koya ambaye amemaliza muda wake. Eng. Rujomba ni mhandisi katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mjini Moshi (MUWSA).
4. **Eng. Leonard Msenyele** ameteuliwa kuwa **Kaimu Mkurugenzi Mtendaji** wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWSA). Eng. Msenyele anachukua nafasi ya Eng. Antony Sanga aliyeteuliwa hivi karibuni kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji. Kabla ya uteuzi huu, Eng. Msenyele alikuwa Meneja wa Miradi katika Mamlaka hiyo.

5. **Bi Joyce Ally Msiru** amehamishwa na kuteuliwa kuwa **Mkurugenzi Mtendaji** wa Mamlaka (mpya) ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya **Same-Mwanga** (Same-Mwanga UWSA). Same-Mwanga UWSA ni Mamlaka mpya ilioanzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 672 la tarehe 23 Agosti 2019, ambayo itahudumia miji ya Same na Mwanga na maeneo mengine yatakayopitiwa na Mradi wa Maji wa Same-Mwanga-Korogwe.
6. **Bw. John Sirati** ameteuliwa kuwa **Kaimu Mkurugenzi Mtendaji** wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mjini Bukoba (BUWASA), akichukua nafasi ya Bw. Allen Marwa aliyehamishiwa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mjini Kahama. Bw. Sirati ni Meneja wa Fedha wa BUWASA.



Prof. Kitila Mkumbo
KATIBU MKUU
Wizara ya Maji
13 Oktoba 2019